SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA

MHE. KHAMIS JUMA MWALIM (MBM)
KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI
KUHUSU MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

MEI, 2019

YALIYOMO

UTANGULIZI 1
Muundo na Majukumu ya Wizara.....3
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019.....5
Mapitio ya Utekelezaji wa Malengo kwa Mwaka 2018/2019....6
G01 – Wizara ya Katiba na Sheria.....6
Taasisi Zinazojitegemea.....15
G02 – Mahakama.....15
G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.....21
G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.....24
G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria.....26
MUELEKEO WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.....28
Vipaumbele vya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2019/2020.....28
G01 – Wizara ya Katiba na Sheria..... 30
G02 – Mahakama.....34
G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.....35
G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.....36
G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria.....36
SHUKURANI 37
HITIMISHO.....38
Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2018/19.....41
Kiambatanisho 2: Muelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.....44
Kiambatanisho 3: Makusanyo ya Mapato kwa Julai-Machi 2018/2019 na Makadirio ya 2019/2020.....48

Kiambatanisho 4: Miradi ya Maendeleo 2019/2020.....49
Kiambatanisho 5a: Muundo wa Wizara ya Katiba na Sheria.....50
Kiambatanisho 5b: G01 – Programu Kuu, Programu Ndogo na Huduma.....51
Kiambatanisho 6a: Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2018/2019.....53
Kiambatanisho 6b: Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama za Mwanzo 2018/2019.....56
Kiambatanisho 6c: Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama za Kadhi 2018/2019.....57
Kiambatanisho 7a: Miswada ya Sheria 2018/19 58
Kiambatanisho 7b: Matangazo ya Kisheria - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu 2018/19.....59
Kiambatanisho 7c: Sheria Ndogondogo - 2018/19.....62
Kiambatanisho 8a: Taasisi Zilizosafirisha Mahujaji 2018 – UTAHIZA..... 64
Kiambatanisho 8b: Taasisi Zilizosafirisha Mahujaji - BAKWATA.66

HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA

MHE. KHAMIS JUMA MWALIM (MBM)
KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia uzima, hekima na afya njema na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kila siku ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima natoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umahiri wake katika kuiongoza vyema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Chini ya uongozi wake, Serikali imetekeleza kwa kiwango kikubwa Ilani ya CCM ya 2015-2020 na ametekeleza kwa kiasi kikubwa ahadi alizozitoa kwa wananchi wa Zanzibar wakati wa Uchaguzi Mkuu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu na afya njema katika kuwahudumia wananchi wa Zanzibar.

Aidha, nachukua fursa hii kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini na kuniteua mimi kuongoza Wizara ya Katiba na Sheria. Ninaahidi kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa uadilifu.

4. **Mheshimiwa Spika,** pongezi zangu za dhati zimwendee Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda, kwa namna anavyomsaidia Rais kutekeleza shughuli mbali mbali za Umma na kusimamia vyema utekelezaji wa Shughuli za Serikali.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwenyekiti wa Kamati ambaye ni Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mfenesini na Makamo wake Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar Mwakilishi wa Viti Maalum wa Vijana Mkoa wa Kusini Pemba kwa kuiongoza vyema Kamati ya Katiba, Sheria na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi. Aidha, nawapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati mbali mbali za Baraza lako Tukufu.

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuishukuru Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Idara Maalum kwa ushauri, maelekezo na ushirikianao mzuri iliotupatia wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa

mwaka wa fedha 2019/2020, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Barazani hotuba hii ya bajeti. Wizara yetu itaendelea kuzingatia ushauri wa Kamati hii wakati tukitekeleza malengo yetu kwa mwaka huu wa fedha.

7. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, naomba kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na Kamati ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuliongoza vyema Baraza letu Tukufu.

8. **Mheshimiwa Spika,** naishukuru familia yangu kwa msaada wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. Shukurani za pekee ziende kwa wananchi wa Jimbo la Pangawe kwa kuendelea kuniamini kuwatumikia na kushirikiana nami katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu. Ushirikiano wao unanipa faraja ya kutekeleza majukumu yangu katika nafasi niliyonayo. Nawaahidi nitaendelea kuwatumikia kwa uwezo wangu wote.

Muundo na Majukumu ya Wizara

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria imeundwa upya mnamo tarehe 3/3/2019, baada ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, kufanya maamuzi ya kuigawa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kufanya Wizara mbili. Wizara nyingine ni Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kutokana na mgawanyiko huo, Wizara ya Katiba na Sheria inayo majukumu yafuatayo: -

i. Kuandaa na kusimamia mipango, sera, sheria na tafiti zinazohusiana na Katiba na Sheria;

ii. Kusimamia shughuli za utawala, uendeshaji na utumishi katika Wizara;

iii. Kusimamia utekelezaji wa Katiba ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

iv. Kusimamia shughuli za Mhimili wa Mahakama;

v. Kusimamia shughuli za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu;

vi. Kusimamia shughuli za Mkurugenzi wa Mashtaka;

vii. Kusimamia shughuli za Tume ya Kurekebisha Sheria;

viii. Kuratibu na kusimamia shughuli za Ofisi ya Mufti;

ix. Kuratibu na kusimamia shughuli za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana; na

x. Kuratibu shughuli za Wizara Pemba.

10. Mheshimiwa Spika, hotuba hii itahusisha Utangulizi ambao tayari nimeshauwasilisha, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti na Malengo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Muelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Shukrani na hatimaye Hitimisho.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

11. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/2019, taasisi zinazounda Wizara ya Katiba na Sheria ziliidhinishiwa shilingi 14,040,900,000.00 kwa kazi za kawaida ambapo makadirio ya mishahara yalikuwa shilingi 8,471,600,000.00 na matumizi mengineyo yalikuwa shilingi 5,569,300,000.00. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, kiasi cha shilingi 10,051,431,691.00 kilipatikana kwa matumizi ya kawaida, zikiwemo shilingi 6,353,178,780.00 za mishahara sawa na asilimia 75 na shilingi 3,698,252,911.00 za matumizi mengineyo, ambazo ni sawa na asilimia 66.

12. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za maendeleo zilitengewa shilingi 500,000,000.00. Kiasi cha fedha za maendeleo kilichopatikana ni shilingi 408,010,000.00 zikiwemo shilingi 178,000,000.00 (36%) kutoka Serikalini na shilingi 230,010,000.00 zilipatikana kupitia mchango wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) katika utekelezaji wa Mradi wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria.

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ruzuku Wizara ilikadiriwa kutumia shilingi 2,102,500,000.00 na hadi kufikia Machi 2019 imepokea shilingi 1,586,120,304.00 sawa na asilimia 75. Kwa upande mwingine, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi 710,499,000.00 na kuchangia mapato ya Serikali. Hadi Machi 2019, fedha zilizokusanywa ni shilingi 408,659,754.00 sawa na asilimia 58 ***(viambatanisho nam. 1&3 vinahusika).***

14. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria inasimamia mafungu matano ambayo ni G01 – Wizara ya Katiba na Sheria; G02 - Mahakama; G03 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu; G04 - Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka; na G05 - Tume ya Kurekebisha Sheria ***(kiambatanisho 5a).***

G01 – Wizara ya Katiba na Sheria

15. **Mheshimiwa Spika,** Fungu G01 lina Programu ya Usimamizi wa Katiba na Sheria; Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara. Yafuatayo ni maelezo kuhusu utekelezaji wa programu hizi tatu ***(kiambatanisho 5b).***

Programu ya Usimamizi wa Katiba na Sheria.

16. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji wa vyombo vya Sheria, Sheria ya Adhabu namba 6/2018 na Sheria ya Mwenendo wa Jinai namba 7/2018 zimeanza kutumika na kuleta tija katika usimamizi wa kesi za jinai ambapo imepunguza malalamiko yanayohusiana na kesi za udhalilishaji na kujenga matumaini kwa jamii. Vile vile, Serikali imetunga Sheria ya Usimamizi wa Mahakama namba 11/2018 *(Court Administration Act)* ambayo kimsingi inaanzisha mfuko wa Mahakama *(Judicial Fund)* pamoja na kutenganisha shughuli za Mahakama na za Kiutawala. Zana hizi ni muhimu katika kuleta ufanisi zaidi wa kiutendaji na usimamizi wa upatikanaji wa haki.

17. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanya tafsiri na kuiweka katika lugha nyepesi Sheria ya Mahakama ya Kadhi, ili iweze kufahamika kwa wepesi. Hatua iliyofikia kwa sasa ni kwamba tafsiri ya Sheria hiyo iko kwa Mpiga chapa kwa ajili ya kutolewa nakala ili zisambazwe kwa wahusika mbali mbali.

18. **Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Msaada wa Kisheria namba 13/2018 imekamilishwa na kupitishwa rasmi na Serikali na Mpango wa Utekelezaji Sera ya Msaada wa Kisheria kwa Kipindi cha miaka mitano umetayarishwa na kuanza kutekelezwa. Kwa kushirikiana na UNDP, Wizara imetayarisha Mradi wa Uwezeshaji na Kuimarisha Upatikanaji wa Haki *(Legal Empowerment and Access to Justice Project - LEAP)* na utekelezaji wake umeanza katika mwaka 2019. Hatua za kutayarisha Skuli ya Sheria ya Zanzibar *(Law School of Zanzibar)* zinaendelea.

19. **Mheshimiwa Spika,** katika kujiandaa na Idara mpya ya Msaada wa Kisheria, tayari matayarisho yamefanyika kwa kupata vitendea kazi na samani kwa msaada wa UNDP. Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria zimeandaliwa, watendaji saba wamefanya ziara ya mafunzo kuhusu msaada wa kisheria Tanzania Bara. Wizara inasubiri uteuzi wa Mkurugenzi ili Idara ianze kufanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria

20. Mheshimiwa Spika, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti imeratibu matayarisho ya kazi mbali mbali zinazoihusu Wizara. Matayarisho ya mpango kazi na bajeti yamefanyika na kuwezesha kukamilisha maandalizi katika wakati uliopangwa. Taarifa za Utekelezaji za robo mwaka, nusu mwaka na taarifa za mwaka zimeandaliwa na kuwasilishwa kunakohusika. Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Sekta ya Sheria umeanza kutayarishwa kwa kuzingatia viashiria vya matokeo vilivyobainishwa katika maandalizi ya bajeti inayotumia PBB. Aidha, elimu imetolewa kuhusu Sera ya Msaada wa Kisheria kupitia mikutano mbali mbali iliyofanyika Unguja na Pemba pamoja na kutoa uelewa kwa jamii kupitia vyombo vya habari. Jumla ya mikutano minne imefanyika.

21. Mheshimiwa Spika, Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji imeratibu vikao vya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji na imefanya kikao kimoja na Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika Sekta ya Katiba na Sheria. Vile vile, kupitia program hii, zimefanyika jitihada za kuhuisha vitengo mbalimbali katika muundo mpya wa Wizara na kujaza nafasi muhimu za wafanyakazi. Idara pia imeratibu ziara za Mheshimiwa Waziri katika Idara na Taasisi za Wizara Unguja na Pemba.

22. Mheshimiwa Spika, Programu Ndogo ya Uratibu wa Wizara Pemba imeendelea kutekelezwa vyema ambapo uratibu wa shughuli za kitaifa umefanyika. Vile vile, kazi za Kamati za Baraza la Wawakilishi pamoja na masuala mengine ya kiutendaji kwa idara na taasisi za Wizara yametekelezwa. Kupitia programu hii pia, Siku ya Sheria, maonesho ya Sheria na Mkutano wa Tume ya Kurekebisha Sheria vimeratibiwa.

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini

23. Mheshimiwa Spika, Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini inatekelezwa kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masuala ya Kiislamu unayozihusu Ofisi ya Mufti wa Zanzibar na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Utekelezaji ni kama ifuatavyo: -

Ofisi ya Mufti wa Zanzibar

24. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mufti wa Zanzibar ina dhamana kisheria ya kuratibu na kusimamia shughuli za Kiislamu zinazoihusu Ofisi ya Mufti kama vile kutoa fatwa, kutatua migogoro ya kijamii na kusimamia miongozo kuhusu masuala ya kidini. Hadi kufikia Machi 2019, Madrasa 133 na misikiti 78 imesajiliwa Unguja na Pemba, kwa lengo la kupata takwimu sahihi za taasisi hizi muhimu kwa jamii. Vile vile, Misikiti 48 na Madrasa 74 zimekaguliwa ili kushauriana na kuhimizana juu ya maendeleo ya taasisi hizo. Aidha, migogoro 14 ya misikiti imepokelewa. Migogoro mitano ya madrasa imetatuliwa na mgogoro mmoja unaendelea kutafutiwa ufumbuzi.

25. **Mheshimiwa Spika,** migogoro katika ndoa na ongezeko la talaka katika jamii yetu ni changamoto kubwa katika familia zetu. Pamoja na juhudi zinazochukuliwa katika utatuzi wa migogoro hiyo lakini bado inaendelea kushamiri. Jumla ya migogoro 193 ya ndoa imepokelewa ambapo miwili inaendelea kutafutiwa ufumbuzi. Pia migogoro 18 ya talaka na kumi ya kijamii imetatuliwa. Migogoro 12 ya mirathi imepokelewa na mmoja unaendelea na utatuzi. Vile vile, masuala 90 yanayohusu ndoa, 101 yanayohusu talaka na 11 ya mirathi yamejibiwa.

26. **Mheshimiwa Spika,** mafunzo ya maadili ya ndoa yanaendelea kutolewa na kwa sasa yapo katika awamu ya tatu. Jumla ya wananchi 134 wamepatiwa mafunzo na kukabidhiwa vyeti na 43 bado wanaendelea kupatiwa mafunzo hayo. Vile vile, Ofisi imetoa mafunzo kwa walimu 144 wa madrasa juu ya kuutumia muongozo kuhusu mbinu bora za kujenga nidhamu ili kupunguza vitendo vya udhalilishaji wa wanafunzi na pia kupunguza matukio ya kutumia adhabu kali za kuumiza mwili.

27. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mufti imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia ZBC Redio. Jumla ya vipindi 96 vya masuala na majibu vimetolewa. Pamoja na hayo vipindi 64 vya nasaha na mawaidha mbali mbali vimetolewa vinavyohusu maadili mema kwa vijana, umuhimu wa kuzidisha uhusiano baina ya dini mbali mbali, umuhimu wa amani na utulivu na umuhimu wa ukweli na uaminifu. Vile vile, mkutano mmoja wa Baraza la Ulamaa umefanyika.

Baraza hili ni chombo chenye jukumu la kumsaidia Mheshimiwa Mufti kutoa fatwa juu ya masuala mazito ya kijamii pale yanapojitokeza.

28. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mufti kwa kushirikiana na kamati ya Zafa Kitaifa imeendelea kuandaa matembezi rasmi ya kidini (Zafa) ya kuukaribisha mwaka mpya wa Kiislamu 1440 Hijria na pia zafa nyengine ilifanyika ya kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W). Sherehe zote hizo ziliwashirikisha walimu na wanafunzi wa vyuo vya Qur-ani, Viongozi mbali mbali wa dini ya Kiislamu nchini, pamoja na waumini kutoka maeneo mbali mbali ya Unguja. Vile vile, Ofisi imeendelea kusimamia Msikiti Mkuu wa Muembeshauri. Aidha, Kamati ya Kitaifa ya Kuthibitisha Kuandama kwa Mwezi imeendelea kuratibiwa ili kupata taarifa sahihi za kuandama kwa mwezi.

29. **Mheshimiwa Spika,** ushirikiano mwema na taasisi nyengine za kidini ndani na nje ya nchi hukuza udugu kwa waumini. Kwa mwaka 2018/19 Ofisi imehudhuria Kongamano la kudumisha Amani Ulimwenguni lililofanyika nchini Uganda. Aidha, Maulamaa wa Zanzibar waliweza kukutana na wenzao wa Tanzania Bara jijini Dares Salam kwa kubadilishana uzoefu na kukuza udugu uliopo. Ofisi pia imepokea wageni kutoka taasisi mbali mbali za kitaifa na kimataifa kama vile UNDP, Save the Children, UNICEF, Faith Associate kutoka UK, na Holistic Education kutoka Uturuki.

30. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mufti ilipokea ugeni wa Waziri wa Shughuli za Kidini wa Saudi Arabia na ilitembelewa na

Mufti wa Jimbo la Cape Town Afrika ya Kusini. Ziara hizo zimezidisha uhusiano baina ya Ofisi ya Mufti wa Zanzibar na taasisi hizo na kuzidi kuitangaza Ofisi hii na kupelekea Mheshimiwa Mufti wa Zanzibar kutembelea nchi mbali mbali kama vile Rwanda, Zambia, Uturuki, Abudhabi na Afrika ya Kusini.

31. Mheshimiwa Spika, ili kujiimarisha kitaaluma, Ofisi imewapeleka masomoni watumishi wawili kwa ngazi ya Shahada ya Uzamili na kuwajengea uwezo watumishi wake ili kuwakumbusha haki na wajibu katika sehemu za kazi. Vile vile, Ofisi imefanikiwa kufanya matengenezo madogo ya jengo la Ofisi na kulipia huduma pamoja na kununua mahitaji muhimu ya Ofisi.

32. Mheshimwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Mufti ilipanga kutumia shilingi 569,300,000.00 kwa matumizi ya kawaida zikiwemo shilingi 306,300,000.00 kwa ajili ya mishahara na shilingi 263,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2019, fedha zilizopatikana ni shilingi 382,531,355.00 (67%) zikiwemo 221,403,855.00 (72%) za mishahara na shilingi 161,127,500.00 (61%) za matumizi mengineyo ***(kiambatanisho nam. 1).***

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

33. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina wajibu wa kusimamia Mali za Wakfu, Amana, Mirathi ya Waislamu, Sala na Mabaraza ya Iddi Kitaifa, Hijja, Zakka

na Misaada ya kheri. Katika mwaka 2018/2019 Kamisheni imeendeleza huduma inazozitoa na kufanikisha utekelezaji wake kama ifuatavyo: -.

34. Mheshimiwa Spika, Kamisheni imeimarisha kumbukumbu na usimamizi wa Mali za Wakfu na Amana na kuongeza tija kwa wanufaika. Mali zote zikiwemo nyumba 312 na mashamba 23 yamekaguliwa mara kwa mara. Kodi ya shilingi 431,796,800.00 imekusanywa na kugaiwa kwa wanufaika. Aidha, shilingi 216,286,036.00 zimetumika kwa kuimarisha nyumba na mashamba. Upatikanaji wa haki za mirathi ni jambo la msingi katika kuleta amani ya familia. Jumla ya tirka 901 zimefunguliwa na tirka 682 zenye thamani ya shilingi 18,730,888,299.30 zimefungwa na warathi kupewa haki zao. Aidha, Kamisheni imetoa ushauri wa kisheria na kushughulikia mashauri 92. Kati ya mashauri hayo 22 yamepatiwa ufumbuzi, 64 yanaendelea na mashauri sita yamepelekwa mahakamani.

35. Mheshimiwa Spika, Sala na Baraza la Idd el Hajj kitaifa limeratibiwa na kufanyika kwa kufana sana katika Wilaya ya Kusini Unguja. Sala ilisaliwa katika Uwanja wa Jamhuri Makunduchi na Baraza lilifanyika katika Ukumbi wa Skuli ya Kizimkazi Mkunguni. Aidha, maandalizi ya Sikukuu na Baraza la Idd el Fitri yatakayofanyika mwezi Juni yameanza.

36. Mheshimiwa Spika, Kamisheni imeendelea kuratibu shughuli za Hijja. Jumla ya mahujaji 1,423 walisafirishwa na Taasisi 19 za Zanzibar kati ya Mahujaji 2,152 waliosafirishwa

na taasisi 27 za Tanzania. Harakati za uanzishaji wa Mfuko wa Hijja zinaendelea ***(Viambatanisho 8a&b vinahusika).***

37. Mheshimiwa Spika, zakka na misaada ya kheri yenye thamani ya shilingi 914,906,000.00 imekusanywa na kugawiwa kwa wananchi wa Unguja na Pemba mijini na vijijini. Zakka na Misaada hiyo ilikusanya fedha taslim Shilingi 5,806,000.00 na chakula chenye thamani ya Shilingi 913,600,000.00.

38. Mheshimiwa Spika: uelimishaji ni jambo linalopewa kipaumbele katika kufanikisha majukumu ya Kamisheni, Jumla ya Vipindi 22 vya Redio na saba vya TV vimerushwa hewani. Aidha, Semina tatu za uelimishaji wa taratibu za mirathi na majukumu ya Kamisheni zimefanyika kwa Masheha wa Wilaya za Mjini, Magharibi A na B. Pia Wananchi 43 wamepatiwa ushauri wa Kisheria na Vipeperushi 955 vimegaiwa.

39. Mheshimiwa Spika: katika mwaka 2018/2019, Kamisheni ilipangiwa kutumia shilingi 968,700,000.00 kati ya fedha hiyo shilingi 548,900,000.00 zilikuwa kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 419,800,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi Machi 2019 shilingi 795,040,850.00 sawa na asilimia 79 zimepatikana. Kati ya fedha hiyo shilingi 433,939,790.00 sawa na asilimia 57 ni mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 361,101,060.00 sawa na asilimia 86 ni matumizi mengine. Aidha, Kamisheni ilikadiriwa kuchangia shilingi 50,589,000.00 katika Mfuko

Mkuu wa Serikali ambapo shilingi 46,423,044.00 (92%) zimepatikana ***(viambatanisho nam. 1&3 vinahusika).***

Taasisi Zinazojitegemea

40. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ina taasisi nne zenye mafungu yanayojitegemea. Kila Fungu lina programu mbili. Programu ya kwanza ni ile inayohusu utekelezaji wa Kazi za Msingi *(Core function)* za taasisi na programu ya pili inahusu utawala na uendeshaji wa ofisi. Fedha zilizomo katika programu hizi zinasimamiwa na Wakuu wa Taasisi husika.

G02 – Mahakama

41. Mheshimiwa Spika, Mahakama ina jukumu la kutafsiri sheria, kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri yote ya jinai na madai yanayowasilishwa mahakamani. Katika kufanikisha jukumu hilo Mahakama imesikiliza kesi mbali mbali za Madai na Jinai pamoja na Rufaa za Mahakama Kuu. Katika kipindi hicho, Mahakama Kuu imepokea mashauri mapya 218 ukijumuisha na mashauri 116 ya nyuma, imekua na mashauri 334 ambapo mashauri 22 yametolewa uamuzi. Divisheni ya kazi ya Mahakama Kuu, imepokea maombi 29 na kufanya Mahakama hiyo iwe na maombi 43 kwa kujumuisha na maombi 14 yaliyosajiliwa kabla. Hadi kufikia Machi 2019, Mahakama hiyo imetoa uamuzi kwa maombi 20.

42. Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Mahakama ya Biashara imepokea mashauri ya madai mapya manne na kufanya iwe na mashauri sita ukijumlisha na mashauri mawili yaliyosajiliwa kabla. Mashauri hayo yote bado yanaendelea kusikilizwa. Mahakama ya Rufaa ya Tanzania katika mwaka wa fedha 2018/2019 ilipokea mashauri 31. Kati ya hayo mashauri manane yalitolewa uamuzi na mashauri 23 bado yanaendelea.

43. Mheshimiwa Spika, katika Mahakama za Mkoa, mashauri mapya 615 yamepokelewa na kufanya Mahakama hizo ziwe na mashauri 889 kwa kujumuisha na mashauri mengine 274 yaliyosajiliwa kabla. Mahakama za Mkoa zimetolea uamuzi mashauri 70. Mahakama za Wilaya zilipokea mashauri mapya 1,141 na kufikisha mashauri 1,511 yanapojumuishwa na mashauri 370 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, mahakama hizo zimetolea uamuzi mashauri 590.

44. Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo zilipokea mashauri mapya 4,891 na kufikisha mashauri 5,092 yanapojumuishwa na mashauri 201 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, Mahakama hizo zimetolea uamuzi mashauri 3,998.

45. Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi wa Rufaa imepokea mashauri mapya 51 na kuifanya iwe na mashauri 82 yanapojumuishwa na mashauri 31 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 22 Kati ya hayo yametolewa uamuzi. Vile vile,

Mahakama za Kadhi wa Wilaya zilipokea mashauri mapya 1,341 na kuwa na mashauri 1,429 baada ya kujumuishwa na mashauri 88 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 830 kati ya hayo yametolewa uamuzi. Mahakama ya Watoto ilipokea mashauri mapya 168 na kufikisha mashauri 228 yanapojumuishwa na mashauri 60 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri yaliyotolewa uamuzi katika Mahakama hiyo ni 25.

46. Mheshimiwa Spika, kulingana na uchambuzi huu, Mahakama imepokea na kusajili mashauri 8,489 katika Mahakama zote kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019. Idadi ya mashauri yaliyosikilizwa na kutolewa uamuzi ni 6,054 sawa na asilimia 71.3. Takwimu hizi zinatuonesha kuwa kuna ongezeko dogo katika usikilizaji na utoaji maamuzi ya kesi ukilinganisha na miaka miwili iliyopita ambapo mwaka 2016/2017 kwa ujumla kesi zilizofunguliwa Mahakama zote zilikua ni 6,953 na zilizotolewa uamuzi zilikua ni 4,753 sawa na asilimia 68.4 na mwaka 2017/2018 kulikuwa na kesi 8,956 kati ya hizo kesi 6,253 sawa na asilimia 70 ***(viambatanisho 6a,b&c vinahusika).***

47. Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama imeendelea na majukumu yake ya kusimamia uajiri, nidhamu na maslahi ya watumishi wa Mahakama. Katika kipindi cha Julai-Machi 2018/2019, Tume imefanya vikao vitatu na kufanya maamuzi juu ya ajira 66, nidhamu tatu na kuthibitishwa kazini watumishi 18. Aidha, Tume imefanya maamuzi ya kuwapandisha vyeo Maafisa Sheria wanne

kuwa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo, Afisa Sheria mmoja kuwa Hakimu wa Wilaya, Mahakimu wa Mwanzo wanne kuwa Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Wilaya sita kuwa Mahakimu wa Mkoa. Aidha, Hakimu wa Mkoa mmoja amepandishwa cheo kuwa Naibu Mrajis.

48. Mheshimiwa Spika, shughuli mbali mbali za Uendeshaji na Utawala wa Mahakama ziliendelea kutekelezwa kama zilivyopangwa. Katika kundelea na lengo lake la kuyafanyia matengenezo majengo yaliyopo na kujenga majengo mapya, tayari hatua za awali za ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu Tunguu zinaendelea kuchukuliwa na matarajio ni kuanza kwa ujenzi huo kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha 2018/2019. Jengo la Mahakama ya Wilaya Mkoani limefanyiwa matengenezo makubwa ikiwemo uwekaji wa paa jipya pamoja na matengenezo ya ukumbi wa Mahakama. Aidha, jengo la Mahakama ya Kadhi Mwanakwerekwe limefanyiwa matengenezo, kuchimba kisima pamoja na kuweka mfumo wa upatikanaji wa maji. Mahakama ya Kadhi pia imeimarisha Uhifadhi wa Kumbukumbu za Mahakama (*Kadhis Court Archive)* na kupatiwa vitendea kazi.

49. Mheshimiwa Spika, ili kuweza kufanikisha upatikanaji wa haki Mahakama imewapatia mafunzo watumishi 60 wa Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalihusu masuala ya kupiga vita rushwa na mafunzo ya kanuni za Utumishi. Mafunzo hayo yalielekezwa kwa Maafisa Sheria, Makarani pamoja na Matarishi. Watumishi wengine watatu

wamepatiwa mafunzo ya ukatibu muhtasi. Pia kulifanyika mafunzo ya lugha za alama kwa Makadhi na Mahakimu wa ngazi mbali mbali. Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwarahisishia kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika utendaji wao. Aidha, watumishi wapya 23 wa Unguja na watatu kutoka Pemba walipatiwa mafunzo elekezi *"Induction Course"* katika Chuo cha Utawala wa Umma Tunguu (IPA).

50. Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Majaji na Mahakimu walishiriki katika mikutano ya ndani na nje ya Nchi ikiwemo Nchi za Afrika ya Kusini, Namibia, Malawi, Nairobi, Uganda, na Tanzania Bara. Aidha, Mhe. Jaji Mkuu alihudhuria Mikutano ya Majaji Nchini Australia, India, China na Misri.

51. Mheshimiwa Spika, Makadhi na Makarani wa Makadhi walipatiwa mafunzo juu ya masuala ya Uchambuzi wa Sheria ya Mahakama ya Kadhi namba 9/2017, Haki za Binaadamu katika Uislamu, taratibu za ufunguaji mashauri katika Mahakama ya Kadhi pamoja na mafunzo ya usuluhishi wa kesi. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa udhamini wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Aidha, kupitia udhamini wa shirika hilo, vyumba viwili vya Mahakama ya Kadhi wa Wilaya Mwanakwerekwe vilifanyiwa matengenezo ili vitumike kama ni sehemu ya kuhifadhia kumbukumbu *(Kadhi's Court Archive).* Vile vile, UNDP imeipatia Mahakama ya Kadhi vitendea kazi ambavyo ni Kompyuta tatu na makabati matano ya kuhifadhia majalada. Zaidi ya hayo kazi ya kutengeneza Kanuni za Mahakama ya Kadhi *(Rules)* inaendelea.

52. Mheshimiwa Spika, Sherehe za kuadhimisha siku ya sheria kitaifa zilifanyika katika Ukumbi wa Baraza la wawakilishi Wete Pemba. Sherehe hizo zilitanguliwa na maonyesho ya siku ya Sheria, yaliyofanyika katika viwanja vya Gombani Chake Chake. Katika maonyesho hayo Taasisi mbali mbali zinazotoa huduma za kisheria zilishiriki kikamilifu.

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2018/2019 Mahakama iliidhinishiwa shilingi 5,611,400,000.00 ambapo kati ya hizo shilingi 4,096,300,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na stahiki na shilingi 1,515,100,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2019, Mahakama iliingiziwa shilingi 4,061,256,903.00 (72%) ambapo fedha za mishahara zilikuwa shilingi 3,063,345,120.00 (75%) na matumizi mengineyo shilingi 997,911,783.00 (66%). Mahakama ya Kadhi ilipangiwa kutumia shilingi 1,113,800,000.00 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini ambapo kati ya hizo shilingi 898,800,000.00 zilitumika kwa mishahara na stahiki na shilingi 215,000,000.00 zilitumika kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2019 Mahakama ya Kadhi iliingiziwa shilingi 777,745,150.00 (70%) ambapo shilingi 651,745,120.00 (73%) zilitumika kwa Mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 126,000,000.00 (59%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 659,910,000.00 zilikadiriwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali. Hadi kufikia mwezi Machi 2019 shilingi 362,236,710.00 (55%) zimekusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ***(viambatanisho nam. 1 & 3 vinahusika).***

G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

54. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ndio Mshauri Mkuu wa Serikali kwa mambo yote ya kisheria. Katika kutekeleza wajibu wake huo Ofisi inatoa ushauri wa kisheria kwa taasisi za Serikali, uandishi wa miswada ya Sheria pamoja na Kanuni za Sheria. Aidha, Ofisi inasimamia kesi na mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali, kuandaa hati na nyaraka za kisheria, kusimamia mikataba yote ambayo Serikali ni sehemu ya mikataba hiyo na kufanya mambo mengine ya kisheria kwa niaba ya Serikali.

55. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji na kuleta ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake, Ofisi imeanzisha muundo mpya na kuwa na Idara badala ya vitengo kama ilivyokuwa awali. Kwa sasa Ofisi ina Idara nne ambazo ni Idara ya Uandishi wa Sheria na Sera za Kisheria, Idara ya Usimamizi wa Kesi za Madai, Idara ya Huduma za Ushauri, Usimamizi wa Mikataba na Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa na Idara ya Mipango, Uendeshaji na Rasilimaliwatu.

56. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma za Sheria Zanzibar, Ofisi ya Mwanasheria imeshughulikia na kuandaa miswada tisa ya Sheria ambayo imewasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa kujadiliwa na hatimae kupitishwa. Miswada yote hiyo imewekwa saini na Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi na sasa Sheria zake zinaendelea kutumika. Kuwepo kwa Sheria hizo kumesaidia kukwamua masuala kadhaa ambayo utekelezaji wake ulihitaji msukumo wa kisheria ***(kiambatanisho 7a kinahusika).***

57. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeandaa Kanuni 13 zinazotokana na Sheria tofauti kwa lengo la kuzifanya Sheria hizo ziweze kutekelezeka kwa ufanisi. Katika kuweka vyema kumbukumbu za kisheria, Ofisi imeandaa Matangazo ya kisheria 54 yanayohusu mambo mbali mbali ambayo yalihitaji kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali na Sheria Ndogondogo ***(viambatanisho 7b&c vinahusika).***

58. Mheshimiwa Spika, katika usimamizi wa mikataba, Ofisi imeendelea kuishauri Serikali juu ya masuala mbali mbali ambayo Serikali ilihitaji kufunga nayo mikataba. Mikataba 268 ilifanyiwa mapitio na kutolewa ushauri na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kati ya mikataba hiyo 38 ni ya ushauri elekezi *(Consultancy)*; 94 ni ya huduma *(Goods and services);* 38 ya ujenzi (Works); 56 ya kodi *(Leases);* na miwili ya ushirikiano *(Joint ventures).*

59. Mheshimiwa Spika, Hati za Maelewano (MoU) 36 zinazohusu Sekta ya Elimu, Afya, Ujenzi, Biashara, Uchumi, Kilimo na Uvuvi zilifanyiwa mapitio na kutolewa ushauri na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Hati hizo za maelewano zimesaidia taasisi husika kufanya kazi kwa ushirikiano na kuleta ufanisi na ujuzi kwa mambo ambayo yanaleta tija kwa

umma na hatimae serikali kufikia malengo ya kuwafikishia wananchi maendeleo. Aidha, kwa upande wa kuiwakilisha Serikali kwenye Mashauri ya Kesi na kutoa ushauri wa kisheria kuhusiana na mashauri hayo, Ofisi imesimamia kesi 87. Katika kesi hizo kesi 11 zimefikia hatua ya kutolewa uamuzi ambapo kati ya hizo kesi tano za Mahakama ya Rufaa na kesi tano Mahakama Kuu Serikali imeshinda. Kwa sasa kesi 76 zinaendelea kusimamiwa zikiwa katika hatua mbali mbali. Aidha, tafiti mbali mbali zimefanyika kwa ajili ya mashauri ya madai ya mahakamani ikiwemo shauri la madai linalohusu uhalali wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lililofunguliwa katika Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Arusha. Katika shauri hilo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar na Bara zinashirikiana katika kuziwakilisha pande mbili za Muungano.

60. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Utawala na Usimamizi wa Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imewajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Watumishi watatu wamesomeshwa katika ngazi ya Shahada ya pili ya Sheria na mfanyakazi mmoja katika ngazi ya shahada ya kwanza ya Sheria. Vile vile, watumishi watano wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kwenye fani mbali mbali. Watendaji wa Idara ya Usimamizi wa Kesi walipata mafunzo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Madai pamoja na Uandishi wa Hati za Madai. Katika kuimarisha mazingira bora ya kazi Ofisi imefanya matengenezo madogo madogo ya jengo.

61. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imenunua na kuweka kamera za kiusalama ili kumalizia sehemu muhimu ambazo kamera zake zilikufa ama hazikuwepo hapo awali kwa dhamira ya kuimarisha ulinzi katika eneo hilo. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imepata Ofisi yake Pemba katika jengo Jipya la Ofisi za Serikali liliopo Gombani. Ofisi inaendelea na taratibu za kuajiri wanasheria na watumishi wa kada nyengine ili kuanza kazi rasmi katika Ofisi ya Pemba katika mwaka wa fedha 2019/2020 mara baada ya kukamilika mchakato wa ajira.

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iliidhinishiwa shilingi 2,027,400,000.00 zikiwemo shilingi 730,200,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 1,297,200,000.00 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana kufikia Machi 2019 ni shilingi 1,399,300,739.00 sawa na asilimia 72 kati ya fedha hizo 560,480,130.000 sawa na asilimia 77 ni kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 838,820,609.00 sawa na Asilimia 65 kwa matumizi mengineyo ***(kiambatanisho nam. 1 kinahusika).***

G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

63. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imesimamia kesi za jinai 1,803 zilizofunguliwa katika mahakama mbali mbali za Unguja na Pemba ambapo kesi 888 zimetolewa uamuzi na kesi 915 zinaendelea katika hatua tofauti. Vile vile, ushirikiano umeimarishwa

baina ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na taasisi nyengine ambazo zinahusika na masuala ya jinai kama vile Mahakama, Magereza, Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Tanzania Bara ili kuhakikisha usimamizi bora wa haki za jinai kwa raia. Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi wa serikali na wahusika wengine kupitia mafunzo kinayoyatoa.

64. Mhesimiwa Spika, kesi mbali mbali zikiwemo kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto, madawa ya kulevya na kesi za uhujumu uchumi zimeshughulikiwa kwa njia maalum ya operesheni ambayo imesaidia kupunguza muda wa ushughulikiaji wa kesi hizo.

65. Mhesimiwa Spika, Ofisi imewapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi sita katika kada ya sheria ngazi ya shahada ya uzamili. Kati ya hao watatu ni wanaume na watatu ni wanawake. Jumla ya wanasheria 11 walihudhuria mafunzo mbali mbali ya muda mfupi ambayo yameongeza ujuzi na taaluma ya kutekeleza vyema majukumu ya kazi.

66. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliidhinishiwa shilingi 2,685,100,000.00 zikiwemo shilingi 1,586,400,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi, na shilingi 1,098,700,000.00 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana ni shilingi 1,781,324,740.00 sawa na asilimia 66. Kati ya fedha hizo 1,226,852,115.00 sawa

na asilimia 77 ni kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 554,472,625.00 sawa na asilimia 50 kwa matumizi mengineyo. Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti kilitengewa ruzuku ya shilingi 20,000,000.00 na fedha zilizopatikana ni shilingi 13,334,334.00 sawa na asilimia 67 ***(viambatanisho nam. 1&3 vinahusika).***

G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria

67. Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea kufanyia mapitio sheria zilizopitwa na wakati na zinazohitaji kuwekwa katika mazingira ya sasa. Tume imekamilisha mapitio ya Sheria nne, ambazo ni Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana namba 2/2007, Sheria ya Mahusiano Kazini namba 1/2005, Sheria ya Ajira namba 11/2005 na Sheria ya Watu Wenye ulemavu (Haki na Fursa Sawa) namba 9/2006. Aidha, mapitio ya awali ya Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai Sura 8/1917 yamefanyika.

68. Mheshimiwa Spika, utafiti na uchambuzi wa matumizi ya Sheria za Zanzibar umefanyika ambapo sheria 100 zilifanyiwa uchambuzi ili kugundua upungufu, matumizi na ubora wa sheria hizo. Kwa upande wa kukuza uwelewa wa jamii kuhusu majukumu, kazi na umuhimu wa mapitio ya sheria, vipindi 25 vya redio na kumi vya televisheni vilirushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC). Vile vile, mikutano imefanyika na kuwashirikisha wahusika mbali mbali katika wilaya zote za Zanzibar na

kuwapa fursa ya kutoa maoni yao juu ya mapitio ya Sheria husika.

69. **Mheshimiwa Spika,** Tume imeendelea kujiimarisha kiutendaji ambapo mafunzo ya kada mbali mbali yametolewa kwa watumishi wote ikiwemo mafunzo kuhusu maadili, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Wanasheria watano walipatiwa mafunzo juu ya kufanya utafiti wa kisheria na uhusiano wa sera na mipango ya maendeleo katika uandishi wa Sheria. Vile vile, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa.

70. **Mheshimiwa Spika,** ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa umeimarika ambapo Tume imeshiriki katika Mkutano wa Jumuiya ya Wanachama wa Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za Afrika Mashariki na Kusini (ALRAESA) na Mkutano wa Jumuiya ya Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola (CALRAs). Vile vile, mkutano mmoja wa ushirikiano kati ya Tume ya kurekebisha Sheria Zanzibar na Tume ya kurekebisha Sheria Tanzania Bara umefanyika.

71. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 Tume ya Kurekebisha Sheria iliidhinishiwa shilingi 1,045,200,000.00 zikiwemo shilingi 304,700,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 740,500,000.00 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana kufikia Machi 2019 ni shilingi 840,897,650.00 sawa na asilimia 80. Kati ya fedha hizo shilingi 195,412,650.00 sawa na asilimia 64

ni kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 645,485,000.00 sawa na asilimia 87 kwa matumizi mengineyo ***(kiambatanisho nam. 1 kinahusika).***

MUELEKEO WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

72. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 sasa naomba kutoa maelezo ya muelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Vipaumbele vya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2019/2020

73. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Katiba na Sheria imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

1. Kuendeleza utekelezaji wa Sera, Sheria na Mipango ya kukuza upatikanaji wa haki ili kuimarisha uchumi wa Taifa. Wizara itaongeza kasi ya kutekeleza Sera ya Msaada wa Kisheria na Sera nyingine za Kitaifa zinazogusa sekta ya Sheria.

2. Kuanza ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu Tunguu ikiwa ni katika vipaumbele vya kitaifa. Jengo la Mahakama Kuu litakapokamilika, litapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la nafasi za Ofisi kwa Mhimili wa Mahakama

na hivyo kuimarisha ufanisi wa kiutendaji. Wizara pia imedhamiria kuendeleza jitihada za kuweka mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa kesi na kuwajengea uwezo Mahakimu na Majaji juu ya matumizi ya mfumo huo. Aidha, Mfumo wa uhifadhi nyaraka na uendeshaji kesi katika Mahakama ya Kadhi utaimarishwa. Katika bajeti hii pia Wizara itahakikisha kuwa majukumu ya Tume ya Utumishi ya Mahakama yanatekelezwa kwa mujibu wa sheria.

3. Kuimarisha uendeshaji wa mashtaka kwa kesi za udhalilishaji wa kijinsia, madawa ya kulevya, makosa ya uhujumu wa uchumi na zile za kawaida;

4. Kuimarisha usimamizi wa mashauri ya madai kwa Mawakili wa Serikali katika masuala ya migogoro ya ardhi;

5. Kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali ili kuweza kushughulikia kiutaalamu makosa ya jinai na madai yanayoibua changamoto kubwa kwa jamii na Serikali;

6. Kuongeza kasi ya kufanya mapitio ya sheria kwa kutoa kipaumbele maalum kwenye Sheria za Ardhi;

7. Kusimamia na kuratibu shughuli za fatwa, mashauri, ushauri wa kidini, taaluma, tafiti, misikiti na madrasa;

8. Kuanzisha rasmi Mfuko wa Hijja na kusogeza huduma za Kamisheni ya Wakfu Wilayani;

9. Kuimarisha uingizaji wa taarifa za rasilimaliwatu katika mfumo wa kielektroniki (HRMIS);

10. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itatekeleza Mradi wa Kuimarisha Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki kwa ushirikiano na UNDP. Mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Taasisi za sheria zisizo za kiserikali; na

11. Kushirikiana na watoa huduma za kisheria walioko nje ya serikali ili kutekeleza vyema dhana ya upatikanaji wa huduma na msaada wa kisheria.

G01 – Wizara ya Katiba na Sheria

74. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa program hii, yafuatayo yatatekelezwa:-

Programu: Usimamizi wa Katiba na Sheria

75. Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha jukumu la utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kufanyika kwa ufanisi, Wizara imekusudia kuanzisha daftari la watoa huduma ya msaada wa kisheria, kuwasajili, ili waweze kutambulika na kufatiliwa utendaji wao pamoja na kuwajengea uwezo maafisa wasimamizi wa utoaji huduma za msaada wa kisheria. Vile vile, mtaala na muongozo wa kufundishia *(curriculum and training Manual)* kwa watoa huduma za

kisheria utaandaliwa na kusambazwa kwa wahusika. Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sheria ya Mahakama ya Kadhi, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Adhabu zitachapishwa kwa lugha nyepesi na kusambazwa kwa wahusika wote ili ziweze kueleweka na kuleta tija kwa walengwa.

76. Mheshimiwa Spika, elimu kwa umma kuhusu masuala ya katiba na sheria itatolewa ili jamii ipate kufahamu mambo ya msingi yanayohusu Katiba pamoja na kushajihisha na kuwezesha utatuzi wa migogoro *(dispute resolution).* Wizara itashiriki katika vikao vya Kitaifa na Kimataifa vinavyohusu masuala ya Katiba, Sheria na Haki za Binaadamu.

Programu: Usimamizi wa Masuala ya Dini

77. Mheshimiwa Spika, programu Ofisi ya Mufti wa Zanzibar imepanga kuratibu na kusimamia shughuli za Kiislamu zinazoihusu Ofisi ya Mufti kama vile kutoa fatwa, kutatua migogoro ya kijamii na kusimamia miongozo kuhusu masuala ya kidini. Ofisi ya Mufti itaimarisha uwezo wake kwa kupata usafiri na kununua jenereta litakalosaidia upatikanaji wa umeme wa dharura. Semina za masuala ya ndoa zitaendelea kutolewa sambamba na kuendelea kusajili misikiti na madrassa.

78. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imeazimia kuanza kutumia kwa majaribio mifumo ya Wakfu, Urithi na Usimamizi wa Kesi. Mifumo hii itaimarisha

huduma, uhifadhi wa kumbukumbu, ufuatiliaji na kudhibiti mwenendo wa majalada. Vile vile, Kamisheni itaimarisha muundo wa kiutendaji ili kuweza kutoa huduma bora na za haraka katika ngazi zote. Kamisheni imepanga kuanza kutayarisha Wakfu wa fedha taslimu na usimamizi wa mirathi kielektroniki. Mfuko wa Hijja utaanza kufanya kazi na vile vile Kamisheni itapeleka huduma zake Wilayani.

Programu: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria.

79. Mheshimiwa Spika, Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria ina programu ndogo tatu na inatekelezwa kupitia Idara ya Utawala na Uendeshaji, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi Kuu – Pemba.

80. Mheshimiwa Spika, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti itaendelea kuratibu na kuandaa mipango na bajeti ya Wizara, kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango katika masuala ya Katiba, Sheria, Usimamizi na upatikanaji wa haki, miradi ya Sekta ya Katiba na Sheria pamoja na kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Wizara. Aidha, Idara itafanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara, kuratibu masuala Mtambuka yanayoihusu sekta ya sheria na kufanya tafiti za Ofisi.

81. Mheshimiwa Spika, Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji imepanga kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili waweze

kutekeleza vyema majukumu yao. Aidha, usalama wa majengo utaimarishwa kwa kuweka vifaa vya kinga wakati wa ajali pamoja na kutoa mafunzo ya afya na usalama wa wafanyakazi pahala pa kazi. Katika kipindi hiki, utaratibu wa kupima utendaji kazi kwa watumishi na uandaaji wa viongozi wa Wizara utatekelezwa. Vile vile, taratibu za matumizi ya miongozo mbali mbali ya kiutumishi ukiwemo utekelezaji wa mkataba wa huduma kwa mtaka huduma itasimamiwa. Kumbukumbu za Watumishi wa Wizara zitaimarishwa kwa kuingiza taarifa zinazokosekana katika mfumo wa kielektroniki. Kupitia Programu hii pia, mfumo wa Usimamizi wa Fedha, Ununuzi, Habari na Ukaguzi wa Ndani itasimamiwa ipasavyo.

82. Mheshimiwa Spika, Programu Ndogo ya Uratibu Shughuli za Wizara Pemba itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuratibu masuala ya Katiba na Sheria, ikiwemo utekelezaji wa Mradi wa Uwezeshaji na Uimarishaji wa Upatikanaji wa Haki kwa upande wa Pemba. Aidha, Ofisi Kuu Pemba itaweka utaratibu muafaka wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji kazi za Wizara kwa upande wa Pemba.

83. Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Fungu G01 liweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 4,397,500,000.00, zikiwemo shilingi 2,514,200,000.00 za matumizi ya kawaida ambapo shilingi 1,250,200,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 1,264,000,000.00 kwa matumzi mengineyo; na shilingi 1,883,300,000.00 za maendeleo

zikiwemo shilingi 400,000,000.00 kutoka Serikalini na shilingi 1,483,300,000.00 kutoka kwa washirika wa maendeleo (UNDP) ***(viambatanisho nam. 2&4).***

84. Mheshimiwa Spika, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya Ruzuku shilingi 1,092,200,000.00, kwa ajili ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Kati ya fedha hizo shilingi 582,100,000.00 ni mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 510,100,000.00 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Fungu G01 linakadiria kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi 82,190,000.00 zitakazokusanywa kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ***(viambatanisho 2&3).***

G02 – Mahakama

Programu: Upatikanaji wa Haki na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

85. Mheshimiwa Spika, Mahakama imejipanga kuendelea na jukumu lake kuu la usikilizaji wa kesi na utoaji maamuzi kwa wakati, kuhakikisha mfumo wa kisasa wa usimamizi wa kesi unaimarika na kuendelea kujenga na kuyafanyia matengenezo majengo ya Mahakama Unguja na Pemba.

86. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 7,849,900,000.00. Kati ya fedha hizo, Mahakama pekee imekadiriwa kutumia shilingi 6,214,400,000.00.

zikiwemo shilingi 4,411,100,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi, na shilingi 1,803,300,000.00 za matumizi mengineyo. Mahakama ya Kadhi imepangiwa kutumia shilingi 1,635,500,003.00 ikiwa ni Ruzuku ambapo shilingi 838,686,660.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 796,813,343.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo. Shilingi 710,310,000.00 zinatarajiwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali ***(viambatanisho 2&3).***

G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Programu: Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

87. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali katika masuala ya kisheria. Katika kipindi hiki, Ofisi itatayarisha miswada ya kisheria, itasimamia utayarishaji wa mikataba, kanuni na matangazo ya kisheria. Uwezo wa Watendaji utaimarishwa kwa kuwapatia fursa za mafunzo na vitendeakazi muhimu.

88. Mheshimiwa Spika, ili Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iweze kutekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa Fedha 2019/2020 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha shilingi 2,114,300,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Shilingi 736,400,000.00 zitatumika kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,377,900,000.00 kwa matumizi mengineyo **(kiambatanisho nam. 2).**

G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Programu: Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Jinai na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

89. Mheshimiwa Spika, Ofisi imepanga kusikiliza kesi za jinai 5,000 katika mahakama mbali mbali za Unguja na Pemba. Ofisi pia imepanga kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi sita katika kada ya sheria ngazi ya shahada ya uzamili. Aidha, huduma na Utawala na Uendeshaji zitatolewa.

90. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 2,869,500,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Shilingi 1,669,900,000.00 zitatumika kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,199,600,000.00 kwa matumizi mengineyo. Aidha, naliomba baraza lako liidhinishe shilingi 20,800,000.00 kama ruzuku ya uendeshaji Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti ***(kiambatanisho nam. 2).***

G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Programu: Mapitio ya Sheria za Zanzibar na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

91. Mheshimiwa Spika, mapitio ya Sheria za Zanzibar yatahusu sheria kumi, ambazo ni Sheria ya Mipango Miji Sura 85/1955, Sheria ya Usajili wa Wathamini namba 5/2015, Sheria ya

Upatikanaji wa Ardhi Sura ya 95/1909, Sheria ya Utambuzi wa Ardhi namba 8/1990, Sheria ya Upimaji wa Ardhi namba 9/1990, Sheria ya usajili wa Ardhi namba 10/1990, Sheria ya Matumizi ya Ardhi namba 12/1992, Sheria ya Uhaulishaji Ardhi namba 8/1994, Sheria ya Kuanzisha Mahakama ya Ardhi namba 7/2008 na Sheria ya Kamisheni ya Ardhi namba 6/2015. Aidha, utafiti na uchambuzi wa matumizi ya Sheria za Zanzibar utafanyika na kuandaa ripoti, Vilevile elimu kwa umma kupitia vipindi vya radio na televisheni, makongamano na semina zitatolewa. Tume itaimarisha utendaji wa kazi za Tume kwa kushirikiana na Taasisi zenye majukumu sawa na Tume kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

92. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Tume ya Kurekebisha Sheria kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 1,090,500,000.00. Kati ya fedha hizo shilingi 320,000,000.00 kwa matumzi ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 770,500,000.00 kwa matumizi mengineyo ***(kiambatanisho nam. 2).***

SHUKURANI

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, nachukua fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza la Wawakilishi. Ninawashukuru Washirika wa Maendeleo waliochangia kwa namna moja au nyingine katika utendaji wa vyombo vya Sheria na vyombo vya Dini Zanzibar.

Miongoni mwao ni: UNDP, Legal Service Facility (LSF), Jumuiya ya Ulaya (EU), UNICEF, Direct Aid (Kuwait), Benki ya Maendeleo ya Kiislam (IDB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Save the Children na Wizara ya Awkaaf ya Algeria. Wizara ya Katiba na Sheria inazishukuru nchi za China, India, Korea, Saudi Arabia, Oman, Uturuki na Egypt. Wizara inatoa shukrani kwa Vyombo vya Sheria vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, tunatoa shukrani kwa Chama cha Wanasheria Zanzibar (ZLS), Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC), na Chama cha Wanasheria Wanawake (ZAFELA); Jumuiya ya Muzdalifa, Jumuiya na Taasisi mbali mbali za kidini vikiwemo Vikundi vinavyosafirisha Mahujaji na taasisi za misaada ya kheri Zanzibar. Sina budi pia kuvishukuru vyombo vya habari kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa elimu na kutangaza matukio mbali mbali yanayohusu shughuli za Wizara ya Katiba na Sheria.

93. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla naomba niwashukuru wote walioisaidia Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuchangia mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yake. Ninamalizia kwa kuwashukuru Watendaji Wakuu na Watumishi wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano wanaonipa.

HITIMISHO

94. Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kueleza kuwa Wizara ya Katiba na Sheria ina msukumo mkubwa kuona kuwa upatikanaji wa haki kwa wananchi unaongezeka. Utekelezaji wa Mradi mpya wa Kuimarisha Uwezeshaji na Upatikanaji

wa Haki umelenga kuweka misingi itakayowezesha serikali kuongeza ufanisi katika kufikia malengo ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020, malengo ya MKUZA III, Dira ya mwaka 2020, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Sherehe za Mapinduzi za mwaka 2019, pamoja na Lengo namba 16 la Maendeleo Endelevu Duniani linalohusu amani, haki, uwajibikaji, taasisi imara, na ushiriki wa wote.

95. Mheshimiwa Spika, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waiidhinishie Wizara ya Katiba na Sheria shilingi 19,434,700,003.00 kutekeleza kazi za kawaida na za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kati ya fedha hizo, shilingi 17,551,400,000.00 ni kwa matumizi ya kawaida ambapo mishahara ni shilingi 9,808,386,660.00 na matumizi mengineyo ni shilingi 7,743,013,343.00. Shilingi 1,883,300,000.00 ni kwa matumizi ya maendeleo zikiwemo shilingi 400,000,000.00 kutoka Serikalini na shilingi 1,483,300,000.00 zinatoka UNDP. Jumla ya fedha za ruzuku ambazo Wizara ya Katiba na Sheria imetengewa ni shilingi 2,748,500,000.00 zikiwemo ruzuku za mishahara shilingi 1,420,786,660.00 na ruzuku za matumizi mengineyo shilingi 1,327,713,340.00. Fedha hizi zimeelekezwa katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Kituo cha Sheria na Utafiti na Mahakama ya Kadhi ***(Viambatanisho 2&4 vinahusika).***

96. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia Baraza lako liikubalie Wizara ya Katiba na Sheria ichangie shilingi 792,500,000.00 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ***(Kiambatanisho nam. 3).***

97. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2018/19

FUNGU/IDARA	JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	MISHAHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA	%	MISHAHARA ILIYOPATIKANA	%	MATUMIZI MENGINEYO ZILIZOPATIKANA	%
Ofisi ya Mufti	569,300,000	306,300,000	263,000,000	382,531,355	67	221,403,855	72	161,127,500	61
Mahakama	5,611,400,000	4,096,300,000	1,515,100,000	4,061,256,933	72	3,063,345,120	75	997,911,783	66
Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	2,027,400,000	730,200,000	1,297,200,000	1,399,300,739	69	560,480,130	77	838,820,609	65
Ofisi ya Mkur. wa Mashtaka	2,685,100,000	1,586,400,000	1,098,700,000	1,781,324,740	66	1,226,852,115	77	554,472,625	50

FUNGU/IDARA	JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	MISHAHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA	%	MISHAHARA ILIYOPATIKANA	%	MATUMIZI MENGINEYO ZILIZOPATIKANA	%
Tume ya Kurekebisha Sheria	1,045,200,000	304,700,000	740,500,000	840,897,650	80	195,412,650	64	645,485,000	87
Ruzuku Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	968,700,000	548,900,000	419,800,000	795,040,850	82	433,939,790	79	361,101,060	86
Ruzuku ya Mahakama ya Kadhi	1,113,800,00	898,800,000	215,000,000	777,745,120	70	651,745,120	73	126,000,000	59

FUNGU/IDARA	JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	MISHAHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA	%	MISHAHARA ILIYOPATIKANA	%	MATUMIZI MENGINEYO ZILIZOPATIKANA	%
Ruzuku DPP	20,000,000		20,000,000	13,334,334	67			13,334,334	67
JUMLA KUU	14,040,900,000	8,471,600,000	5,569,300,000	10,051,431,691	72	6,353,178,780	75	3,698,252,911	66
JUMLA G01	569,300,000	306,300,000	263,000,000	382,531,355	67	221,403,855	72	161,127,500	61
G02 -G05	**1,369,100,000**	**6,717,600,000**	**4,651,500,000**	**8,082,780,032**	**71 %**	**5,046,090,015**	**75 %**	**3,036,690,017**	**65 %**
JUMLA YA RUZUKU	**2,102,500,000**	**1,447,700,000**	**654,800,000**	**1,586,120,304**	**75%**	**1,085,684,910**	**75 %**	**500,435,394**	**76 %**
G01-G05	**11,938,400,000**	**7,023,900,000**	**4,914,500,000**	**8,465,311,387**	**71 %**	**5,267,493,870**	**75%**	**3,197,817,517**	**65%**

Kiambatanisho 2: Muelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA				KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
G02-Mahakama	6,214,400,000	4,411,100,000	1,803,300,000				6,214,400,000
G03-Ofisi ya M/Mkuu	2,114,300,000	736,400,000	1,377,900,000				2,114,300,000
G04-Ofisi ya M/Mashtaka	2,869,500,000	1,669,900,000	1,199,600,000				2,869,500,000
G05-Tume ya K/Sheria	1,090,500,000	320,000,000	770,500,000				1,090,500,000

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA				KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
G01-Idara ya Uendeshaji na Utumishi	916,819,400	523,126,000	393,693,400				916,819,400
G01-Ofisi Kuu Pemba	401,065,600	238,149,000	162,916,600				401,065,600
G01-Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	396,285,000	111,895,000	284,390,000	400,000,000	1,483,300,000	1,883,300,000	2,279,585,000
G01-Ofisi ya Mufti	800,030,000	377,030,000	423,000,000				800,030,000
G01-Ruzuku KWNMA	1,092,200,000	582,100,000	510,100,000				1,092,200,000

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA				KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
G02-Ruzuku Mahakama ya Kadhi	1,635,500,003	838,686,660	796,813,343				1,635,500,003
G04-Ruzuku Ofisi ya M/Mashtaka	20,800,000		20,800,000				20,800,000
Jumla ya Ruzuku G01	**1,092,200,000**	**582,100,000**	**510,100,000**				**1,092,200,000**
Jumla ya Ruzuku G02-05	**1,656,300,000**	**838,686,660**	**817,613,340**				**1,656,300,000**
Jumla ya Ruzuku	**2,748,500,000**	**1,420,786,660**	**1,327,713,340**				**2,748,500,000**

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA				KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
Vote G01	2,514,200,000	1,250,200,000	1,264,000,000	400,000,000	1,483,300,000	1,883,300,000	4,397,500,000
Jumla G01& Ruzuku G01	3,606,400,000	1,832,300,000	1,774,100,000	400,000,000	1,483,300,000	1,883,300,000	3,606,400,000
Vote G02- G05	12,288,700,000	7,137,400,000	5,151,300,000	-	-	-	12,288,700,000
Jumla G1 - G5	14,802,900,000	8,387,600,000	6,415,300,000	400,000,000	1,483,300,000	1,883,300,000	16,686,200,000
Jumla Kuu	17,551,400,000	9,808,386,660	7,743,013,340	400,000,000	1,483,300,000	1,883,300,000	19,434,700,000

Kiambatanisho 3: Makusanyo ya Mapato kwa Julai-Machi 2018/2019 na Makadirio ya 2019/2020

Kifungu	Idara /Taasisi	Makadirio 2018/2019	Makusanyo Halisi	%	Makadirio 2019/2020
G01	**G01 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana**	50,589,000.00	46,423,044.00	92	82,190,000.00
G02	**G02 Mahakama**	659,910,000.00	362,236,710.00	55	710,310,000.00
G04	**G04 Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti**	100,000,000.00	92,373,000.00		90,000,000.00
	Jumla	810,499,000.00	501,032,754.00	62	882,500,000.00
	Zinazoingizwa Mfuko Mkuu wa Serikali	**710,499,000.00**	**408,659,754.00**	**58**	**792,500,000,00**

Kiambatanisho 4: Miradi ya Maendeleo 2019/2020

Namba ya Mradi	Jina la Mradi	Mchango wa Serikali	Washirika wa Maendeleo	Maelezo/Jumla
	Ujenzi wa Jengo la Mahakama Kuu Tunguu			Fedha za Mradi huu zimewekwa Wizara ya Fedha na Mipango katika Mradi wa Ujenzi Ofisi za Serikali
00000P006	Mradi wa Kuimarisha Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki (LEAP)	400,000,000	1,483,300,000	Mradi huu unafadhiliwa na UNDP
	Jumla Kuu	**400,000,000**	**1,483,300,000**	**1,883,300,000**

Kiambatanisho 5a: Muundo wa Wizara ya Katiba na Sheria

Wizara ya Katiba na Sheria inaundwa na Idara na Taasisi zifuatazo: -

i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;

ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;

iii. Ofisi Kuu Pemba

iv. Ofisi ya Mufti;

v. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana;

Wizara pia inasimamia Taasisi za Sheria zinazojitegemea ambazo ni: -

vi. Mahakama Kuu

vii. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

viii. Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

ix. Tume ya Kurekebisha Sheria

Taasisi za Wizara ambazo zinapokea Ruzuku ni: -

x. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

xi. Chuo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti

xii. Mahakama ya Kadhi

Kiambatanisho 5b: G01 – Programu Kuu, Programu Ndogo na Huduma

Programu	Programu Ndogo	Huduma
1. Programu ya Usimamizi wa Katiba na Sheria	1.Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utoaji Huduma za Kisheria	1. Kuratibu Masuala ya Kisheria 2.Kuratibu na Kutoa Msaada wa Kisheria
2. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini	1.Programu Ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masuala ya Kiislamu	1. Kuratibu na Kusimamia Misikiti, Madrassa, Taasisi na Masuala ya Kidini
		2.Usimamizi wa Mirathi, Wakfu, Amana, Zakka na Shughuli za Kiislamu
3. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria	1.Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji	1. Uendeshaji na Usimamizi wa Rasilimaliwatu Katika Wizara

Programu	Programu Ndogo	Huduma
	2.Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti	2. Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti 3.Uratibu wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo
	1. Uratibu wa Wizara Pemba	4.Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

Kiambatanisho 6a:- Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2018/2019

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahakama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Mahakama ya Rufaa Tanzania	31					24	8	7	0
M/Kuu Vuga	173	57	7	16	2	52	8	48	5
M/Kuu Pemba	45	2	0	13	0	20	0	10	0
Mahakama ya kazi	29	29	14	0	0	0	0	0	0
Mahakama ya Biashara	4	4	0	0	0	0	0	0	0
M/Kadhi Rufaa Z	49	0	0	0	0	49	20	0	0
M/ Kadhi Rufaa P	2	0	0	0	0	2	2	0	0
M/ Mkoa Vuga	328	6	1	306	32	14	0	2	0
M/Mkoa Mfenesini	70	3	1	65	17	1	0	1	0

Kiambatanisho 6a:- Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2018/2019

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahakama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Mkoa Mwera	82	3	1	78	6	0	0	1	0
Mkoa Wete	31	0	0	31	8	0	0	0	0
Mkoa Chake	104	1	0	97	4	0	0	6	1
Wilaya Mw/kwe	363	21	6	342	155	0	0	0	0
Wilaya Mwera	126	5	4	121	94	0	0	0	0
Wilaya Mkokotoni	79	3	1	76	68	0	0	0	0
Wilaya Mfenesini	90	1	0	89	38	0	0	0	0
Wilaya Makunduchi	68	3	1	65	48	0	0	0	0
Wilaya Mkoani	130	22	9	108	76	0	0	0	0
Wilaya Chake	127	3	1	123	34	1	0	0	0

Kiambatanisho 6a:- Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2018/2019

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahakama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Wilaya Wete	91	3	0	88	19	0	0	0	0
Wilaya Konde	67	0	0	67	36	0	0	0	0
Watoto Vuga	120	83	7	37	6	0	0	0	0
Watoto Chake	20	0	0	20	3	0	0	0	0
Watoto Wete	11	0	0	11	3	0	0	0	0
M/Watoto Mahonda	17	3	1	14	5	0	0	0	0
Jumla	**2,257**	**252**	**54**	**1,767**	**654**	**163**	**38**	**75**	**6**

Kiambatanisho 6b:- Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama za Mwanzo 2018/2019

Ufunguaji wa Kesi Mahakama za Mwanzo					
Mahakama ya Mwanzo		**Kesi za Madai**		**Kesi za Jinai**	
	Jumla	**Zilizo funguliwa**	**Zilizo amuliwa**	**Zilizo funguliwa**	**Zilizoamuliwa**
Manispaa Malindi	1060	0	0	1060	1058
Manispaa Chakechake	0	0	0	0	0
M/kwerekwe	1923	41	21	1882	1770
Mwera	199	36	18	163	157
Mfenesini	498	4	0	498	470
Mkokotoni	286	18	12	268	250
Makunduchi	72	4	3	68	63
Chwaka	1	1	0	0	0
Mkoani	247	14	4	233	205
Kengeja	11	3	1	8	3
Chake chake	345	31	5	314	231
Wete	166	20	5	146	129
Konde	83	6	4	77	63
Jumla	**4,891**	**178**	**73**	**4,713**	**4,399**

Kiambatanisho 6c:- Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama za Kadhi 2018/2019

Ufunguaji wa Kesi Mahakama za Kadhi		
Mahakama za Kadhi Wilaya	**Kesi za Madai**	
	Zilizofunguliwa	**Zilizotolewa uamuzi**
M/Kwekwe	662	366
Mwera	66	5
Mfenesini	106	67
Mkokotoni	82	63
Makunduchi	23	20
Chwaka	0	0
Mkoani	61	60
Kengeja	9	5
Chakechake	193	168
Wete	81	29
Konde	58	47
Jumla	**1341**	**830**

Kiambatanisho 7a: Miswada ya Sheria 2018/19

Miswada
1. Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali.
2. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Matractor.
3. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar 2018.
4. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Vyama vya Ushirika Nam. 4 ya mwaka 1986 na Kutunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar yam waka 2018.
5. Mswada wa Sheria ya Msaada wa Kisheria 2018.
6. Mswada wa Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Zanzibar 2018.
7. Mswada wa Sheria ya Adhabu ya Zanzibar.
8. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.
9. Mswada wa Sheria ya Fedha.

Kiambatanisho 7b: – Matangazo ya Kisheria - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu 2018/19

Matangazo ya Kisheria
1. Presidential Pardon.
2. Uteuzi wa Washauri wa Mahakama.
3. The Online Content Regulations, 2019.
4. Tangaazo la Majina ya Viongozi wa Umma.
5. The Crew List Regulations.
6. The Carriage of Dangerous Goods Regulations.
7. The Limitation of Liability for Maritime Regulations.
8. The Inquiry of Conduct of Seafarers Regulations.
9. The Dec Cargo Regulation.
10. The Bulk Cargo Regulations.
11. Rules for Marine Inquiry and Formal Investigations.
12. The Marine Navigations AIDS Regulations.
13. Regulations for Prevention of Marine Oil Pollutions.
14. The Seafarers Medical Examinations 2018.
15. The Official Log Book Regulations.
16. The Prevention of Collision and Disaster Signal Regulations.
17. The Port Reception Facility for Ship-Generated Wastes and Cargo Residues.

Matangazo ya Kisheria
18. The Repatriations and Reef.
19. The Safe Manning Regulations.
20. The Seafarers Engagement Regulations.
21. The Small Ships Regulations.
22. The Stowaway Regulations.
23. The Timber Cargo Regulations.
24. The Tonnage Measurement Regulations.
25. The Wreck and salvage service Regulations.
26. Publication of the Muster Plan.
27. Appointment of Deputy Principal Secretaries.
28. Appointment of Principal Secretaries.
29. Appointment of the Deputy Minister.
30. Appointment of the Minister.
31. Appointment of the Regional Magistrate.
32. Appointment of Primary Magistrate Court.
33. The Survey and Certifications Regulation.
34. Appointment of the Member of the Public Commission.
35. Appointment of the Chairman of Board of Directors Zanzibar Airports Authority.

Matangazo ya Kisheria
53. The Closer of Road from KWA JUMA PWEZA TO SAATEN.
54. The Closer of the road from Magogoni (Al-Tabibu Hospital) to Kikosi cha Zimamoto at Mwanakwerekwe.
55. Appointment of the Chairperson of the Land Transfer Board.
56. Appointment of the Chairperson of the Board of Director – Zanzibar Petroleum Upstream Regulatory Authority.
57. Appointment of Deputy Vice Chancellor for Administratio of the State University of Zanzibar.
58. Appointment of Deputy Vice Chancellor for Academics of State University of Zanzibar.

Kiambatanisho 7c: Sheria Ndogondogo - 2018/19

Sheria Ndogondogo
1. The Crew List Regulations.
2. The Carriage of Dangerous Goods Regulations.
3. The Limitation of Liability for Maritime Regulations.
4. The Inquiry of Conduct of Seafarers Regulations.
5. The Dec Cargo Regulation.
6. The Bulk Cargo Regulations.
7. The Marine Navigations AIDS Regulations.
8. Regulations for Prevention of Marine Oil Pollutions.
9. The Seafarers Medical Examinations 2018.
10. The Official Log Book Regulations.
11. The Prevention of Collision and Disaster Signal Regulations.
12. The Safe Manning Regulations.
13. The Seafarers Engagement Regulations.
14. The Small Ships Regulations.
15. The Stowaway Regulations.

Sheria Ndogondogo
16. The Timber Cargo Regulations.
17. The Tonnage Measurement Regulations.
18. The Wreck and salvage service Regulations.
19. The Survey and Certifications Regulation.
20. Consumer Complaints Handling Procedures Regulations, 2018.
21. The Business Entity Registration Regulations, 2018.
22. The Secured Transaction on Movable Property Regulations, 2018.
23. Kanuni za KMKM za Uchunguzi na Ukamataji, 2018.
24. Kanuni za Kudumu za Mabaraza ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2018.

Kiambatanisho 8a: Taasisi Zilizosafirisha Mahujaji 2018 – UTAHIZA

Taasisi	Maombi	Halisi
1. Ahlusunna waljamaa Hajj & Umra Trust	100	70
2. Albir Hajj, Umra & travelling Agency	60	80
3. Al firdaus Hajj Group	51	65
4. Alnoor Hajj & Travelling Agency	50	25
5. Alsafaa Hajj & Umra Trust	100	60
6. Alharamain Development Foundation	80	110
7. Aljazeera Hajj, Umra & Travelling Agency	80	70
8. Haj Caravan Group	55	60
9. Ikram Hajj & Travelling Agency	60	90
10. Labayka Hajj, Umra and Trav.Agency	50	29
11. Tahfidh Hajj Group	50	30
12. Talbiya Hajj, Umra and Travelling Agency	50	0

Taasisi	Maombi	Halisi
13. Taufiq Hajj and Travelling Agency	50	50
14. Tawheed Development Network	150	100
15. Tatwawwue Hajj & Travelling Agency	70	70
16. Zanzibar Imams Association	90	115
17. Zadaawa Hajj & Travelling Agency	80	70
18. Zanzibar Istiqama Hajj & Trav. Agency	120	126
19. Zanzibar Hajj & Travelling Agency	120	103
20. Zanzibar Istiqama Charitable Organisat.	120	100
Jumla	**1,606**	**1,423**

Kiambatanisho 8b: Taasisi Zilizosafirisha Mahujaji - BAKWATA

	Taasisi	Maombi	Halisi
1.	Ahlu Daawa Hajj & Travelling Agency	170	178
2.	Albushra Tours	70	-
3.	Al Husnaa Hajj Trust	55	55
4.	BAKWATA	150	120
5.	Hajj Khidmat		-
6.	Ibnu Taymiah Salaf Foundation	50	-
7.	Masjid Adil	100	80
8.	Peace Travel	80	80
9.	Shamsul Maarif	50	-
10.	Shifaa Hajj	216	216
11.	Tabazat Babu Salaam	50	-
12.	Tanzania Charitable Development Org,	81	-
13.	Tanzania Muslim Development Association	50	-
Jumla		**1,172**	**729**